MTANDAO WA MAENDELEO YA WATOTO WADOGO TANZANIA

TANZANIA EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT NETWORK

(TECDEN)

KATIBA YA MWAKA 2008

1. Usuli.

KWA KUWA Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania ulizaliwa mnamo Desemba 2000, kufuatia mfululizo wa mikutano ya asasi za malezi ya watoto wadogo ya kimaTaifa iliyojumuisha serikali na asasi zisizo za serikali ili kujadili ushiriki wa Tanzania katika mpango wa Chuo Kikuu Huria sehemu ya chuo Kikuu cha Victoria Canada (ECDVU) kuhusiana na Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.

KWA KUWA ushirikiano huu wa wadau wa taasisi za serikali na zisizo za serikali katika Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo ulibainisha malengo manane ambayo yangeweza kusaidia Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania, mojawapo ikiwa ni "kuanzisha na kuendeleza mtandao hai wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo kupitia muungano wenye nguvu wa asasi zinazojishughulisha na makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.

KWA KUWA kile kilichoanza kama kamati ya ushirikiano miongoni mwa taasisi kiligeuka na kuundwa Mtandao wa Kitaifa usio rasmi wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania ukiwashirikisha wadau kutoka serikalini na asasi zisizo za kiserikali.

KWA KUWA miongoni mwa malengo ya kuanzishwa kwake kwa wakati huo ilikuwa ni kuimarisha mfumo wa kitaifa wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo, kwa kutandaa, kubadilishana taarifa, kukuza uelewa na utetezi kwa nia ya:

- Kushawishi utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo.
- Kuongoza harakati za Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo
- Kuchangia katika utengenezaji wa mitaala na mafunzo ya Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.
- Kuchangia katika kuzijengea uwezo asasi za kijamii (CBOs)
- Kukuza uhusiano wa sekta mbalimbali
- Kuchunguza, kutafiti, kutunza kumbukumbu na kusambaza taarifa.

- Kufanya miradi ya majaribio ya ubunifu na usoefu wa asasi za kijamii kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto, kutunza kumbukumbu za uzoefu huo na kusambaza taarifa zake ili kushawishi ukuaji wa sekta kwa baadae.
- Kuwa kiungo kwa sekta za kiwizara za mipango ya maendeleo.

KWA KUWA baadhi ya mafanikio ya Mtandao ni pamoja na:

- Mwaka 2001 rasimu ys Tanzania ya Malezi, Makuzi Na Maendeleo Ya Watoto Wadogovu ilikubaliwa na miongoni mwa shughuli za mwanzo za Mtandao ilikuwa ni kupendekeza washiriki wanne katika mpango huo. Wote wanne walikubalika na kuingizwa kwenye mpango huo.
- Tarehe 5 Septemba 2001, ulifanikisha majadiliano yenye kichwa cha habari "kuelekea njia ya pamoja kwa ajili ya, Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania" yaliyohusisha wadau muhimu ikiwa ni pamoja wawakilishi wa ngazi za juu toka wizara tatu zinazojihusisha na masuala ya Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.
- Desemba 2001 Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ilichukua uongozi katika kuratibu masuala ya Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo na hatua hiyo iliungwa mkono na wanachama wa Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo na kuifanya Wizara hii kuwa muitishaji wa mikutano kuhusiana na masuala yaliyo chini ya mwavuli wa Mtandao.
- Februari 2002:
    - Kamati mpya ya kusaidia uratibu iliteuliwa ambayo ilijumuisha wawakilishi wa ngazi za juu toka serikalini, sekta za afya, elimu, ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii pamoja na mashririka ya Umoja wa Mataifa na asasi zisizo za kiserikali.
    - Ujumbe wa kamati ya uratibu ulishiriki katika mkutano wa kikanda wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo uliofanyika Mombasa na kudhaminiwa na Bernad Van Leer Foundation.

- Agosti 2002 Wizara ya Elimu na Utamaduni ilipokuwa inatayarisha taarifa kwa ajili ya mkutano wa MINEDAF VIII kuhusu maendeleo yaliyopatikana kwenye malengo ya Elimu kwa Wote (EFA) Mtandao ulifanikiwa kushawishi mratibu wa EFA kuungana na Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo katika kukubaliana na ukweli kwamba Tanzania ilikuwa bado haijashughulikia lengo la kwanza la EFA, malezi ya awali ya watoto na elimu.
- Septemba 2002, mkutano wa wadau wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo na EFA ulifanyika na kuhudhuriwa na uwakilishi mpana kutoka sekta mbalimbali na wadau wengine.
    - Kikundi cha kazi Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo EFA kiliundwa kwa ajili ya kutayarisha mpango wa utekelezaji wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.
- Oktoba 2002:
    - Ulifanikisha kufanyika kikao maalum wakati wa mkutano wa MNEDAF VIII pamoja na kutengeneza nyenzo za ushawishi na mkakati kwa kutandaa kimkoa, kitaifa na kimataifa.
    - Kushiriki katika mkutano wa mipango wa mfuko wa elimu wa jumuia ya madola (CEF), ambapo matokeo yake suala la Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo liliwekwa miongoni mwa vipaumbele.
- Desemba 2002, kufanikishaji kufanyika kikao maalum cha Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo na ushawishi kwa njia nyingine katika MINEDAF VIII.
- Februari 2003:
    - Utayarishaji wa waraka wenye kichwa cha habari “Tanzania Kuelekea Mpango wa Utekelezaji Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo na EFA 2003-2015” ulikamilika na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya mrejesho.

- Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ilikubali kuteua kauli mbiu ya Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo wakati wa maadhimisho ya sherehe ya siku ya mtoto wa Afrika ya mwaka 2003.

- Juni 16, 2003 kauli mbiu ya siku ya mtoto wa Afrika "Malezi Bora ya Utotoni ni Msingi kwa Maisha", ilikubalika na asasi mbalimbali kama ni fursa ya utetezi nchini kote.

- June 24-25 2003- Mkutano wa Taifa wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo ulihudhuriwa na washiriki 83 kutoka sekta zenye kuhusiana na Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo, taasisi zisizo za kiserikali, pamoja na washirika katika maendeleo, ya kitaifa na kimataifa. ulijadili muswada wenye kichwa cha habari "Tanzania kuelekea Mpango wa Utekelezaji, Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo EFA 2003-2015''

- Mkutano huo ulikuwa ni tukio muhimu kwa Tanzania na ulifungua njia katika ufuatiliaji wa kina kwa:

  i) Kuteua kamati ya muda kutayarisha mapendekezo kwa ajili ya kamati ya uratibu ya Mtandao na wanachama wake kuhusu:

     - Kuratibu mitazamo tofauti iliyofungamanishwa Katika sekta mbali mbali kuhusu Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania

     - Kuunda Mtandao huru nje ya serikali lakini wenye uhusiano na serikali kimkakati.

  ii) Kuwa na sekretarieti yenye wanachama wa Mtandao kutoka Morogoro, Mwanza, Moshi na Iringa ambao walikuwa mstari wa mbele Katika uanzishaji wa mitandao ya Maendeleo ya Watoto Wadogo katika ngazi ya mkoa kwenye sehemu zao ili kuhakikisha kuwa Mtandao una uwakilishi kutoka ngazi ya jamii hadi Taifa.

  - Septemba 2003 maombi ya Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo kwenye Mfuko wa Elimu ya Jumuiya ya Madola kuhusu mpango mkakati wa Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto

Wadogo hatua ya kwanza Septemba 2003 hadi Januari 2004 yalipitishwa. Kipindi cha Mpango kilikuwa ni Septemba 2003 – Machi 2004.

- Oktoba 2003 mfuko wa elimu wa Jumuiya ya Madola ulipitisha ufadhili wa kikundi cha wanawake cha safina Morogoro kwa miezi miwili ili kupanga na kusaidia kufanikisha mkutano wa zaidi ya washiriki 80, uliofanyika tarehe 11 had 12 Novemba na kupitisha kuanzishwa kwa Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Morogoro kama tawi la Mtandao wa kitaifa.
- Februari 2004 tathmini ya hali ya Mtandao ilikamilishwa na ambayo ilitumika kama hadidu za rejea Katika kikao cha kutafakari hali ya mtandao kilichofanyika kuanzia tarehe 19 hadi 21 Februari.

KWA KUWA pamoja na mafanikio hayo, kuna changamoto zilizotanabaishwa ambazo zinaweza kuhusishwa moja kwa moja na ile hali ya Mtandao kutokuwa rasmi. Nazo ni: -

(i) Kutokuwa na njozi, utume, malengo, na maadili ya kiutendaji ya Mtandao

(ii) Kutokuwa na mfumo thabiti na madhubuti wa uongozi na utawala wenye majukumu na wajibu unaoeleweka kwa;

a. Wanachama

b. Kamati ya kuratibu

c. Sekretarieti

d. Vikundi vya kazi.

(iii) Kutokuwa na uwiano wa uwakilishi wa wadau katika Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo kutoka ngazi ya jamii hadi Taifa.

(iv) Kutokuwepo kwa sekretarieti huru ya kudumu yenye kujitosheleza kiraslimali.

(v) Ukosefu wa raslimali kugharamia shughuli mbalimbali za Mtandao.

(vi) Mtandao kutokuwa na hadhi kisheria.

Mkutano uliofanyika Juni 2003 kutafakari na kujadili mswada wa mpango wa utekelezaji wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo EFA wa Tanzania (2003-2015) pia ulichukua fursa hiyo kutafakari hali ya Mtandao na hasa changamoto zilizoainishwa hapo

juu na jinsi ya kuuimarisha. Matokeo yake iliundwa kamati ya muda ishirikiane na kamati ya uratibu iliyokuwepo wakati huo pamoja na **Amani** ECCD (ambayo ilikuwa ikikaimu kazi za sekretarieti ya Mtandao) kutayarisha mapendekezo ya kuimarisha mifumo ya uongozi na utawala ya Mtandao. Kuanzia hapo mikutano mingi na mashauriano yalifanyika na kusababisha kuwepo kikao cha kutafakari Februari 19-21, 2004 kukusanya na kutathmini masuala mbalimbali na uzoefu uliopatikana ili kufanikisha mpango wa utekelezaji unaolenga kuundwa kwa Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo wenye nguvu na usio tegemezi kwenye maamuzi pamoja na sekretarieti iliyo huru. Na katiba hii ni matokeo ya kikao hicho.

KWA HIYO BASI KATIBA HII IMETUNGWA NA MTANDAO WA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA WATOTO WADOGO, kwa niaba ya wanachama wote kwa madhumuni ya kujenga Mtandao na kuhakikisha kwamba Mtandao huo unaongozwa kwa kufuata misingi ya demokrasia, haki na usawa.

1.0 IBARA YA KWANZA: Jina, nembo na anwani ya mtandao

Jina la Mtandao huu litakuwa "Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania" au kwa Kiingereza utaitwa "Tanzani Early Childhood Development Network" au kwa kifupi utaitwa "TECDEN".

Makao Makuu ya mtandao yatakuwa Dar es Salaam na utafanya shughuli zake nchi nzima, Tanzania bara na Zanzibar.

1.1 Nembo

i. Mtandao utakuwa na nembo ya kuutambulisha.

ii. Nembo ya mtandao itaonesha ramani ya Tanzania, picha ya mtoto mdogo na jina la mtandao

iii. Nembo hiyo itatumika kwenye karatasi za barua na nyaraka nyingine za Mtandao,

iv. Nembo ya mtandao itatumika katika ngazi zote za Taifa na Mikoa.

1.2: Lakiri

i. Kutakuwa na lakiri ya Mtandao itakayokuwa na jina la "**Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania**" likiwa limeandikwa kwa herufi kubwa na itakuwa na nembo inayoutambulisha Mtandao.

ii. Lakiri hiyo itakuwa na umbile la duara na itapigwa kwenye nyaraka zote za kisheria mbele ya mwenyekiti wa kamati Elekezi ya Taifa au makamu wake na mjumbe mmoja wa kamati Elekezi ya Taifa.

2.0 IBARA YA PILI: Tafsiri ya Maneno

Katika katiba hii, isipokuwa itakapoelezwa vingenevyo, manaeno yafuatayo yatatafsiriwa kama ifuatavyo:

i. **Mtandao** ni Mtandao wa Makuzi, Malezi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania

ii. **Mtoto** ni mtoto wa mwanadamu kuanzia mimba hadi umri wa miaka nane (0-8)

iii. **Serikali** ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ngazi zake zote.

iv. **Zanzibar** ni visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vinavyovizunguka visiwa hivyo.

v. **Maendeleo ya mtoto** ni huduma zote zinazolenga kumuendeleza mtoto katika kupata haki zake za kuishi, kulindwa, kupata malezi, kupendwa, uchangamshi, ushirki na elimu ya awali ili kumuhakikishia makuzi bora tangu mimba hadi miaka minane (0-8).

vi. **Mkoa** ni sehemu ya eneo la nchi kama inavyotafsiriwa na serikali.

vii. **TECDEN** (*Tanzania Early Childhood Development Network)* Mtandao wa Malezi Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo.

viii. **MKUKUTA-** Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umaskini Tanzania.

2.0 IBARA YA TATU: Uwepo wa kisheria.

Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania (TECDEN) Ulisajiriwa rasmi tarehe 30 June, 2004 na msajili wa mashirika wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi chini ya sheria ya asasi za jamii (Societies Ordinance) ya Mwaka 1954.

2.1 Mtandao una mamlaka ya:

i. Kumiliki mali zisizohamishika na zinazohamishika.

ii. Kushitaki na kushitakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

iii. Kuingia mikataba

iv. Kuhawilisha mali chakavu.

v. Kutafuta na kupokea misaada kutoka ndani na nje ya nchi.

vi. Kutoa huduma bila faida

4.0 IBARA YA NNE: Walengwa

i. Walengwa wakuu wa mtandao ni watoto wote wa Tanzania tangu mimba hadi umri wa miaka minane.

ii. Wadau wote wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kabla ya mimba hadi umri wa miaka minane.

5.0 IBARA YA TANO: Dira, Dhamira na Malengo ya mtandao.

5.1.0: Dira

Dira ya mtandao ni kuwa na Tanzania yenye watoto wanaopatiwa huduma bora za makuzi, malezi na maendeleo kwa ujumla wake.

5.2.0: Dhamira

Mtandao umedhamiria kufikia dira yake kwa kuhakikisha kuwa wanachama wote wa Mtandao wanafanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine ili kuendeleza mkabala

wa kuunganisha sekta zote husika ambazo zinatilia mkazo maendeleo jumui ya mtoto na ambazo zinaakisi haki na sauti za watoto wadogo katika masuala yanayowahusu.

5.3.0: Lengo Kuu

Lengo kuu la mtandao huu ni kujenga mazingira bora yatakayo imarisha uwezo wa wanachama katika ngazi zote ili waweze kushiriki kikamilifu katika michakato muhimu ya uandaajisera na utekelezaji mipango jumui ya maendeleo ya watoto ili kuwa na sauti ya pamoja.

5.3.1 Malengo Mahsusi

Mtandao una malengo mahususi yafuatayo:

i) Kuwahamasisha wadau juu ya umuhimu wa mkabala jumui katika maendeleo ya mtoto.

ii) Kutafuta raslimali watu, vifaa na fedha kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha maendeleo ya watoto wadogo.

iii) Kuendeleza na kujenga uwezo wa wanachama wa mtandao wanaojishughulisha kikamilifu na masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya watoto.

iv) Kujenga utamaduni madhubuti wa upashanaji na ubadilishanaji taarifa zinazohusu masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya watoto katika ngazi zote.

v) Kurahisisha kuwepo kwa mtiririko wa mawasiliano ya haraka na madhubuti miongoni mwa wanachama wa mtandao katika ngazi zote.

vi) Kuwa mstari wa mbele katika kushawishi mabadiliko ya sera, miongozo na sheria zinazohusu haki na maendeleo ya watoto wadogo kwa kushiriki kikamilifu katika ushawishi na utetezi.

vii) Kutoa mapendekezo, kufanya na/au kuwezesha kufanyika tafiti na uchambuzi juu ya masuala yanayohusu malezi, makuzi na maendeleo ya watoto kwa nia ya kusambaza na/au kuhifadhi taarifa.

viii) Kushirikiana na mitandao mingine inayojishughulisha na masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya watoto katika ngazi ya kikanda, kibara na kimataifa.

ix) Kuhamasisha malezi bora ya kijamii.

6.0 IBARA YA SITA: Uanachama (Aina, sifa, ukomo, kusita, kusitishwa)

6.1.0: Aina za uanachama

Mtandao utakuwa na wanachama wa aina mbili zifuatazo:

6.1.1: Uanachama wa Asasi/jumuiya/ mashirika

6.1.2 Unachama wa heshima

6.2.0 Sifa za uanachama

Sifa za uanachama zitatofuatiana kulingana na uanachama wenyewe

6.2.1 Uanachama wa Asasi /jumuiya/mashirika.

Asasi, jumuiya au mashirika yoyote ya kitaifa itakuwa mwanachama wa mtandao kama itakuwa na sifa zifuatazo:

a. Kuthibitisha uwepo wake kisheria, anwani na mahali ofisi ilipo.
b. Kujishughulisha kikamilifu na kazi za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo.
c. Kuthibitisha kwamba asasi inajishughulisha kwa dhati na maswala ya watoto wadogo.
d. Kutojishughulisha na masuala ya kisiasa,
e. Kutokuwa mshirika wa chama chochote cha siasa.
f. Kutambuliwa na kukubalika na jamii ilipo/inapofanya kazi.
g. Kuwa tayari kuheshimu na kufuata katiba ya Mtandao

6.2.3 Uanachama wa heshima

Uanachama huu atatunukiwa mtu binafsi kutokana na mambo yafuatayo:

a) Awe ni mtu mwenye kupenda na kuguswa na masuala ya watoto wadogo.
b) Awe anakubalika na kuheshimika katika Jamii.
c) Awe tayari kukubali malengo madhumuni ya Katiba hii.

d) Awe ameonyesha nia ya kuusaidia Mtandao kufikia Malengo yake kama yalivyoainishwa katika katiba hii.

6.2.4: Utaratibu wa Maombi ya Uanachama

a. Wanachama wa asasi, jumuiya na mashirika ya kitaifa watalazimika kujaza fomu za kujiunga na mtandao zitakazotolewa na kuziwasilisha kwa Kamati Elekezi katika ngazi husika.

b. Kuwa mwanachana wa mitandao ya Mikoa wanamotoka ilimradi wanatimzia masharti yote ya uanachama wao katika ngazi husika.

6.2.5: Wajibu na Haki za Wanachama

6.2.5.1: Wajibu

Kila mwanachama wa Mtandao atakuwa na majukumu ya kufanya ili kuuwezesha mtandao kutimiza madhumuni yake kama ifuatavyo:

a. Kulipa kiingilio na ada ya kila mwaka na michango mingine yoyote itakayoamuliwa na mkutano mkuu.

b. Kulipa michango mingine yoyote kama itakavyoamuliwa na ngazi husika.

c. Kuheshimu na kulinda katiba na kutekeleza kwa ukamilifu kanuni na/au miongozo mbali mbali kama itakavyotolewa na mamlaka husika,

d. Kujenga mtandao na kuendeleza ufanisi na ustawi wake kwa:

    i. Kuwa na ushiriki hai katika mikutano mbali mbali na kujituma kwa dhati katika ufuatiliaji na utekelezaji wa shughuli anuai za mtandao,

    ii. Kushiriki kwa dhati katika kudumisha mawasiliano ya pande mbili na ubadilishaji habari na wanachama wengine wa mtandao katika ngazi mbali mbali,

    iii. Kushiriki kikamilifu katika kazi za pamoja za mtandao kama vile vikundi vya kazi maalumu, na shughuli nyinginezo kama zitavyokuwa zimejitokeza katika mpango mkakati utakaoandaliwa.

6.2.5.2: Haki

Kila mwanachama wa Mtandao atakuwa na haki zifuatazo:

i. Kupatiwa taarifa zote juu ya Mtandao,

ii. Kupiga na kupigiwa kura katika ngazi husika,

iii. Kusikilizwa kwenye shauri lolote husika na kuheshimiwa,

iv. Kushiriki kwenye suala/mkutano wowote unaomhusu,

v. Kujengewa uwezo kwa manufaa ya mtandao pale inapowezekana.

vi. Kutoingiliwa kati kwa masuala yake ya ndani au ya asasi yake.

vii. Kukata rufaa kwenye ngazi husika.

6.3.0: KUKOMA NA KUREJESHEWA UANACHAMA

6.3.1: KUKOMA UANACHAMA

Uanachama kwenye Mtandao utakoma kukitokea chochote kilichotajwa hapa chini kulingana na aina ya uanachama:

i. Kifo kwa mwanachama wa heshima.

ii. Kichaa cha kudumu kilichothibitishwa kisheria kwa mwanachama mmoja mmoja kwa wanachama wa heshima.

iii. Kutolipa ada ya mwaka ya uanachama kwa miaka miwili mfululizo.

iv. Kutohudhuria bila udhuru mikutano mitatu mfuliulizo ya kikatiba au shughuli nyingine zilizotolewa katika ngazi zote.

v. Kutenguliwa na/au kukoma usajili wa asasi, jumuiya na mashirika

vi. Kujitoa kwa maandishi; na/au,

vii. Kufukuzwa/kuachishwa kwa maandishi kutokana na mwenendo usiofaa kulingana na Katiba.

viii. Taasisi/asasi/shirika ikibadilika jina na shughuli zake mbali na zile zilizotajwa wakati wa usajiri.

6.3.2: Kurejeshewa Uanachama

a. Mwanachama yeyote ambaye uanachama wake utakoma kwa mujibu wa kifungu 6.3.1 (iii,iv na v) atarejeshewa uanachama wake endapo tu:

    i. Sababu zake kwa maandishi za kwa nini anataka kujiunga tena na mtandao zitajadiliwa na kukubaliwa na mkutano mkuu wa mtandao katika ngazi husika,

    ii. Atakubaliana na kutekeleza masharti yoyote yatakayotolewa na mkutano mkuu kwa kutegemea sababu za kuachishwa kwake.

b. Mwanachama yeyote ambaye uanachama wake utakuwa umekoma kwa mujibu wa kifungu 6.3.1 (vii) atarejeshewa uanachama wake baada ya:

    i. Kutimiza kifungu (i) na (ii) hapo juu,

    ii. Atamaliza kipindi cha uchunguzi wa mwaka mmoja cha uanachama wa muda bila kufanya makosa.

c. Mwanachama yeyote ambaye uanachama wake utakoma kwa mujibu wa kifungu 6.3.1 (iv) cha katiba hii atarejeshewa uanachama baada ya kutimiza masharti ya kifungu kidogo (i) cha 6.3.2 (a) hapo juu.

7.0 IBARA YA SABA: Muundo wa Mtandao (Mkutano mkuu, Kamati Elekezi, Sekretariati)

Mtandao utakuwa na ngazi tatu dhahiri za mamlaka katika uhusiano, umiliki na kazi:

7.1.0 Mkutano Mkuu wa Taifa

i. Hiki kitakuwa ni chombo chenye mamlaka ya juu kabisa kwenye Mtandao chenye uamuzi wa mwisho katika masuala yote yanayouhusu mtandao.

ii. Utakasimu baadhi ya mamlaka yake kwa Kamati Elekezi ya Taifa kwa masuala yanayohitaji maamuzi na utekelezaji wa haraka.

7.1.1: Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:

i. Wajumbe wote wa Kamati Elekezi ya Taifa,

ii. Wawakilishi wawili kutoka kila mtandao hai wa Mkoa kwa miaka mitatu mfululizo.

iii. Wageni waalikwa kutoka serikalini, mashirika ya maendeleo n.k kama itakavyoamuliwa na Kamati Elekezi ya Taifa.

7.1.2: Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na kazi kuu zifuatazo:

i. Kupitia na kuthibitisha taarifa za fedha na hesabu za mtandao katika ngazi husika, zilizokaguliwa

ii. Kupitia, kuthibitisha na kupitisha sera, mipango mkakati na bajeti,

iii. Kuthibitisha katiba na marekebisho yatakayofanywa baada ya hapo,

iv. Kuthibitisha na/au kusitisha wanachama wa Mtandao kwenye ngazi ya kitaifa, kuthibitisha wanachama wa mikoa mpya iliyokamilisha sifa za kujinga na mtandao.

v. Kuthibitisha na kusitisha wajumbe wa Kamati Elekezi ya Taifa,

vi. Kupanga viingilio, ada na michango mbalimbali.

vii. Kupokea mapendekezo na maoni kutoka kwenye mtandao ngazi za mikoa kuyajadili na kuyatolea maamuzi.

viii. Kumchagua Mwenyekiti wa kusimamia uchaguzi mkuu

ix. Kumchagua Mwenyekiti wa TECDEN Taifa na makamu wake pamoja na wajumbe wa Kamati Elekezi ya Taifa watakaodumu kwa miaka mitatu

7.2.0: Kamati Elekezi ya Taifa

i. Hiki ndicho kitakachokuwa chombo cha uElekezi cha Mtandao ngazi ya Taifa.

ii. Itawakilisha makundi mbalimbali ya uanachama wa Mtandao.

iii. Kwa kadiri inavyowezekana, ujumbe wa kamati Elekezi ya Taifa utazingatia usawa wa jinsia.

iv. Itakasimu mamlaka yake ya kazi za kila siku kwa sekretarieti ya Taifa

7.2.1: Sifa/vigezo vya Ujumbe wa KamatiElekezi ya Taifa

Wajumbe wa kamati hii watapendekezwa na matawi wanachama. Wajumbe walioteuliwa watatakiwa kuchaguliwa kwa kura na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kuwa katika nafasi hiyo kwa miaka mitatu. Wajumbe wanaweza kuchaguliwa tena lakini si kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo. Ili mtu achaguliwe kuwa mjumbe kwa Kamati hii ni lazima:

i. Awe na/au utaalamu/ujuzi/uzoefu katika maeneo ya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto ikiwa ni pamoja na elimu, afya na lishe, , haki za watoto, uchangamshi na michezo, pamoja na uelewa wa masuala mtambuka.

ii. Awe anatoka katika asasi/shirika/taasisi mwanachama inayotekeleza masuala ya malezi makuzi na maendeleo ya watoto wadogo mwenye uwezo wa kufanya maamuzi.

iii. Awe na uwezo wa kushauri, kuchangia maamuzi kwa uhuru na hata kuchangia maendeleo ya mtandao wake bila kushinikizwa na mwajiri au asasi anayotoka

iv. Awe na uwezo wa ushawishi na utetezi na moyo wa kujitolea katika masuala ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto mdogo kama yalivyotajwa katika ibara ya 7.2.1 (i),

v. Awe na mifano halisi ya ushiriki hai katika masuala ya malezi makuzi na maendeleo ya mtoto mdogo, kwenye ngazi ya taifa na kijamii.

vi. Awe na moyo wa kuchangia, kujitolea na utayari wa kufanya kazi kwa bidii na kwa muda mrefu

vii. Awe na uwezo wa kuongea na kuandika Kiswahili na/au Kiingereza kwa ufasaha.

viii. Atambuliwe na mwajiri wake kuwa katika Kamati Elekezi ya Taifa.

ix. Awe na ufahamu wa kutosha kuhusu katiba ya mtandao

7.2.2: Wajumbe wa Kamati Elekezi ya Taifa

Kamati Elekezi ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:

i. Wajumbe saba (7) wenye uwezo wa kupiga kura kupitisha maamuzi watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mtandao Taifa kwa kuzingatia demokrasia. Kati ya wajumbe hao wawepo wajumbe wasiopungua wawili kutoka Zanzibar

ii. Mratibu wa Sekretariati ya Taifa

iii. Wajumbe waalikwa kutegemeana na umuhimu

7.2.3: Kazi za Kamati Elekezi ya Taifa

i. Itafanya kazi zote za Mtandao kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa Taifa na itawajibika kwake,

ii. Itakuwa na mamlaka ya kuajiri na kutengua ajira za watumishi wa sekretatiati yaTaifa.

iii. Kamati Elekezi itafanya kazi chini ya Mwenyekiti au Makamu wake ambao watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

iv. Kuongoza katika uandaaji wa mipango mkakati katika ngazi ya Taifa

v. Kuchambua kwa kina mipango ya muda mrefu, miradi na bajeti za mtandao na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa uthibitisho.

vi. Kupitia na kuhakiki taarifa mbalimbali za fedha na hesabu zilizokaguliwa kabla ya kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa kwa uthibitisho na kuhakikisha miongozo iliyotolewa inafuatwa na Mtandao.

vii. Kupanga na kurekebisha viwango vya ada ya kiingilio na uanachama za kila mwaka na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kujadiliwa na kupitishwa.

viii. Kujadili na kupitisha mipango ya Taifa ya muda mfupi, miradi na bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

ix. Kufuatilia, kusimamia na kusaidia utekelezaji wa mipango, miradi na shughuli za Mtandao ngazi ya Taifa.

x. Kupokea na kupitia maombi ya wanachama wapya yatakayowasilishwa na mitandao ya mikoa na kutoa uanachama wa muda wakati wa kusubiri uthibitisho wa Mkutano Mkuu,

xi. Kupitia sera, kanuni na taratibu zinazohusu masuala mbalimbali ya Mtandao na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa kwa uthibitisho.

xii. Kuteua na kuthibitisha wakaguzi wa mahesabu wa Mtandao ngazi ya Taifa,

xiii. Kusaidia uundwaji wa vikundi vya kitaalam vya utekelezaji kutoka miongoni mwa wanachama wa Mtandao kwa kuzingatia suala mahsusi kama litakalovyojitokeza katika mpango mkakati wa mtandao au suala lolote jingine kama itakavyoonekana inafaa na kutengeneza hadidu za rejea kwa kila kikundi katika ngazi ya Taifa.

xiv. Kutafuta raslimali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zote za Mtandao.

xv. Kuwezesha kuwepo kwa mpango wa kujenga uwezo wa wanachama wote katika ngazi mbali mbali za Mtandao ili kutekeleza kwa ufanisi dira, dhamira na malengo ya mtandao na mipango mkakati mahsusi,

xvi. Kuongoza ushiriki hai wa mtandao katika michakato jumui ya kiTaifa kuhusu:

a. Sera, miongozo na sheria zinazohusu maendeleo ya mtoto mdogo,

b. Kufanya utetezi na ushawishi kwa serikali na wahisani

c. Utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya mtandao na shughuli za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo kwa ujumla.

xvii. Kubaini na kutekeleza masuala yanayohitaji ushauri (kuajiri washauri, kupitia na kuthibitisha taarifa zao) katika ngazi ya Taifa,

xviii. Kuwa na jukumu la msingi katika utafiti, uchambuzi, usambazaji habari na hifadhi ya nyaraka na kuanzisha kitengo cha habari,

xix. Kuwezesha ushiriki hai wa wanachama wa Mtandao kwenye ngazi zote, kwa kuanzisha utaratibu wa mawasiliano ya pande mbili na upashanaji habari.

xx. Kujaza nafasi za Kamati Elekezi ya Taifa zitakazoachwa wazi kwa niaba ya Mkutano Mkuu.

7.3.0: Sekretarieti ya Taifa

i. Hiki kitakuwa chombo cha kusaidia uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Mtandao zitakazofanywa na wanachama wote na kitawajibika kwa Kamati Elekezi ya Taifa,

ii. Itaongozwa na Mratibu mwenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya malezi,makuzi na maendeleo ya watoto wadogo, kutandaa na ushirikiano wa kisekta katika ngazi zote pamoja na ujuzi na uzoefu katika uongozi

iii. Mratibu atasaidiwa kazi zake na wakuu wa vitengo watakaoajiriwa kulingana na mahitaji na uwezo wa mtandao.

iv. Mratibu atakuwa pia ndiye Katibu wa Kamati Elekezi ya Taifa pamoja na mkutano mkuu wa Taifa asiye na haki ya kupiga kura,

v. Maafisa wote wa sekretarieti ya Taifa watalipwa mishahara kulingana na utaalamu wao.

7.3.1 Kazi za Sekretarieti ya Taifa

Sekretarieti ya Taifa itafanya kazi zifuatazo:

i. Kuunganisha wanachama walio kwenye ngazi zinazofanana na ngazi zinazotofautiana na kuwezesha mawasiliano ili kurahisisha mtiririko wa habari miongoni mwa mitandao ya mikoa na wa Taifa,

ii. Kubuni na kuandaa mipango mkakati, programu na miradi ya kitaifa itakayowasilishwa kwenye Kamati Elekezi ya Taifa kwa ajili ya ushauri, kuboreshwa na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa ili kupitishwa na kuthibitishwa,

iii. Kutayarisha taarifa za fedha za benki kwa ajili ya ukaguzi na kuziwasilisha kwenye Kamati Elekezi ya Taifa ili kuzipitia, kuzichambua na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa kwa uthibitisho,

iv. Kusimamia sera, taratibu na kanuni zinazohusu masuala mbalimbali ya Mtandao (ikiwa ni pamoja na fedha) na kuziwasilisha kwenye Kamati Elekezi ya Taifa kwa uchambuzi na kupelekwa mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa kwa ajili kuthibitishwa.

v. Kutekeleza mipango ya kila mwaka na mingineyo, programu na miradi/huduma kama itakavyoamuliwa,

vi. Kutengeneza bajeti na kusimamia fedha za utekelezaji wa shughuli za kila siku za mtandao. ,

vii. Kuandika na kuziweka pamoja taarifa kutoka mitandao ya mkoa na Taifa kwa ajili ya kuzihifadhi na kuweka kumbukumbu,

viii. Kusimamia na kukagua fedha na vifaa vyote vya mtandao ngazi ya Taifa,

ix. Kuitisha vikao vyote vya kamati Elekezi ya Taifa na Mikutano Mikuu ya Taifa baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa mwenyekiti wa Kamati Elekezi ya Taifa na pia kutunza mihutasari, taarifa na nyaraka zote,

x. Kuhakikisha kwamba raslimali zote za Mtandao zinasimamiwa na kutumiwa ipasavyo kulingana na sera, kanuni na taratibu za Mtandao,

xi. Kuhakikisha kuwa vitabu vyote vya hesabu vya Mtandao kwenye ngazi ya Taifa vinatunzwa ipasavyo.

7.4.0: Mkutano Mkuu wa Mkoa

i. Hiki kitakuwa ni chombo chenye mamlaka ya juu kabisa kwenye Mtandao ngazi ya mkoa na chenye uamuzi wa mwisho katika masuala yote ya mtandao katika ngazi hiyo.

ii. Utakasimu baadhi ya mamlaka yake kwa Kamati Elekezi ya mkoa kwa masuala yanayohitaji maamuzi na utekelezaji wa haraka.

7.4.1: Wajumbe wa Mkutano wa Mkoa

Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa wazi kwa:-

i. Mtu yeyote ambaye anaweza akawa mzazi, mtu mashuhuri, mfanyabiashara, n.k. mkaazi wa mkoa husika baada ya kutimiza ibara 6.2.1 (a) – (g), 6.2.4 na 6.2.5 za katiba hii,

ii. Asasi au shirika lolote lililopo katika mkoa husika baada ya kutimiza ibara ya 6.2.1 na 6.2.4 za katiba hii.

iii. Mwakilishi wa kitengo/idara/kurugenzi yoyote ya serikali katika ngazi ya mkoa kama itakavyoamriwa na Kamati Elekezi ya Mkoa.

7.4.2: Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa

Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa na kazi kuu zifuatazo:

Kupitia na kuthibitisha taarifa za fedha na hesabu zilizokaguliwa katika ngazi ya mkoa,

i. Kupitia, kuthibitisha na kupitisha sera, mipango mkakati na bajeti ya mkoa,

ii. Kupendekeza kwa mkutano mkuu wa Taifa marekebisho yoyote ya katiba utakayoona ya lazima,

iii. Kuthibitisha na kusitisha wanachama wa Mtandao kwenye ngazi ya mkoa,

iv. Kuchagua na kusitisha wajumbe wa Kamati Elekezi ya mkoa,

v. Kuchagua wajumbe wawili wa kuwakiisha mkoa katika mkutano mkuu wa Taifa kwa kipindi cha miaka mitatu.

7.5.0: Kamati Elekezi ya Mkoa

i. Hiki ndicho kitakachokuwa chombo cha uElekezi cha Mtandao ngazi ya mkoa,

ii. Itafanya kazi zote za Mtandao ngazi ya mkoa kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa mkoa na itawajibika kwake,

iii. Itakasimu baadhi ya mamlaka yake hasa kuhusiana na kazi za kila siku kwa sekretarieti ya mkoa,

iv. Itawakilisha makundi mbalimbali ya uanachama wa Mtandao katika mkoa,

v. Kwa kadiri inavyowezekana, ujumbe wa Kamati Elekezi ya mkoa itazingatia usawa wa jinsia.

7.5.1: Sifa/vigezo vya Ujumbe wa Kamati Elekezi ya Mkoa

Wajumbe wa Kamati hii watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa mkoa na kushika hiyo ya uongozi kwa miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa tena lakini si kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo. Ili mtu achaguliwe kuwa mjumbe kwa Kamati hii ni lazima:

i. Aonyeshe utaalamu na/au ujuzi kwenye mmojawapo au maeneo yote makuu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo kama malezi ya watoto, utambuzi na urekebishaji wa mapema wa watoto wenye mahitaji maalumu, lishe, usafi wa mazingira, afya, uchangamshaji, michezo na elimu ya awali, VVU/UKIMWI.

ii. Awe na uwezo wa ushawishi na utetezi na moyo wa kujituma katika masuala ya Malezi,Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo mkoani,

iii. Awe na mifano halisi ya ushiriki hai katika masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo kwenye ngazi mbalimbali, k.m. uundaji sera na utekelezaji, uwezeshaji, n.k.

iv. Awe na moyo wa kujitolea na awe tayari kufanya kazi kwa bidii na kwa muda mrefu

v. Itafaa zaidi akiwa na uwezo wa kuongea Kiingereza na Kiswahili kwa ufasaha.

vi. Awe na kibali na kutambuliwa na mwajiri wake kuwa anashiriki katika Kamati Elekezi ya mkoa; na kazi za Kamati Elekezi hiyo ziingizwe kwenye majukumu yake ya kazi.

7.5.2: Wajumbe wa Kamati Elekezi ya Mkoa

Kamati Elekezi ya mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:

i. Wajumbe wasiozidi saba (7) wenye uwezo wa kupiga kura wanaotokana na mashirika/asasi zinazojishughulisha na kazi za malezi, makuzi ya watoto wadogo katika mkoa husika watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa kidemokrasia. Aidha uchaguzi wa wajumbe uzingatie uwiano wa kijinsia.

ii. Mratibu wa Sekretariati ya Mkoa

iii. Wajumbe waalikwa

7.5.3: Kazi za Kamati Elekezi ya Mkoa

Kamati Elekezi ya mkoa yoyote itafanya kazi zifuatazo:

i. Kuifanya sauti ya familia, jamii na wadau wa malezi,makuzi na maendeleo ya watoto wadogo mkoani isikike katika ngazi zote za upangaji na ugawanyaji rasilimali katika masuala ya malezi,makuzi na maendeleo ya watoto wadogo,

ii. Kuunganisha watoto, familia na jamii katika kata na mkoa juu ya masuala anuai ya malezi,makuzi na maendeleo ya watoto wadogo,

iii. Kuweka utaratibu wa kurahisisha mawasiliano na upashanaji habari, ushauri au mazungumzo ya moja kwa moja miongoni mwa wanachama kwa kufuata mfumo wa mawasiliano ulio rasmi na usio rasmi,

iv. Kuwawezesha wanchama kuwa na ushiriki hai katika mikutano, warsha, n.k. katika mkoa, kata na kijiji,

v. Kuanzisha na kushawishi masuala/huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo kwa wazazi, watoto, asasi na vikundi vya kijamii,

vi. Kujenga uwezo na kutoa msaada kwa wazazi, vikundi na asasi za kijamii zinazo jihusisha na utekelezaji wa shughuli za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo mkoani,

vii. Kuratibu shughulu za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo katika mkoa,

viii. Kuwezesha ushiriki wa wanachama katika shughuli za kuzinga na kuzengea kwenye ngazi ya jamii na mkoa ili kushawishi mabadiliko na kutathmini ufanisi wake,

ix. Kusaidia uundwaji wa vikundi vya kitaalam vya utekelezaji kutoka miongoni mwa wanachama wa Mtandao kwa kuzingatia suala mahsusi kama litakalovyojitokeza katika mpango mkakati wa mtandao wa mkoa au suala lolote jingine kama itakavyoonekana inafaa na kutengeneza hadidu za rejea kwa kila kikundi,

x. Kutengeneza mipango mkakati ya muda mrefu, miradi na bajeti na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mkoa kwa ajili ya kuipitia na kuithibitisha,

xi. Kutafuta na kusimamia raslimali kwa ajili ya shughuli za Mtandao katika ngazi ya mkoa,

xii. Kusimamia na kutathmini shughuli/huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo katika mkoa,

xiii. Kuandaa na kuandika taarifa ya utekelezaji na taarifa ya hesabu za fedha iliyokaguliwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa mkoa kwa kupitishwa,

xiv. Kutafuta njia bora za ushirikiano na halmashauri za wilaya,

xv. Kutandaa na mitandao mingine iliyopo katika mkoa,

xvi. Kutafuta wataalam na/au kushirikiana nao au vinginevyo katika kufanya utafiti, uchambuzi, usambazaji, na utunzaji taarifa kwa ajili ya kupashana habari na wadau wengine na kuanzisha kitengo cha habari,

xvii. Kujaza nafasi yoyote itakayoachwa wazi katika Kamati Elekezi ya mkoa,

xviii. Kuteua na kuthibitisha mkaguzi wa hesabu za mtandao katika mkoa,

xix. Kupokea na kupitia maombi ya wanachama wapya ngazi ya mkoa na kutoa uanachama wa muda wakati wa kusubiri uthibatisho wa Mkutano Mkuu wa mkoa,

xx. Kuwa na jukumu la moja kwa moja la kuajiri sekretrarieti ya mkoa.

7.6.0: Sekretarieti ya Mkoa

i. Hiki kitakuwa chombo cha uwezeshaji wa uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Mtandao zitakazofanywa na wanachama wote wa mkoa na kitawajibika kwa Kamati Elekezi ya mkoa,

ii. Itaongozwa na mratibu mwenye historia katika masuala ya Malezi,Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo pamoja na uzoefu na ujuzi katika menejimenti,

iii. Mratibu atasaidiwa kazi zake na wakuu wa vitengo na wafanyakazi wengine,

iv. Mratibu atakuwa ndiye Katibu wa Kamati Elekezi ya Mkoa pamoja na mkutano mkuu wa mkoa asiye na haki ya kupiga kura,

v. Maafisa wote wa sekretarieti ya mkoa watalipwa mishahara kulingana na utaalamu wao na hawatakuwa wa kuchaguliwa na mamlaka yoyote,

7.6.1: Kazi za Sekretarieti ya Mkoa

Sekretarieti ya mkoa itafanya kazi zifuatazo:

i. Kuunganisha wanachama walio kwenye ngazi zinazofanana na ngazi zinazotofautiana na kuwezesha mawasiliano ya pande mbili na kurahisisha mtiririko wa habari miongoni mwa wanachama ndani ya mkoa na baina ya mkoa na mikoa mingine na Taifa,

ii. Kusaidia katika kubuni na kuunda mipango mkakati ya mkoa, programu na miradi itakayowasilishwa kwenye Kamati Elekezi ya mkoa kwa ajili ya ushauri, kuboreshwa na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa mkoa kwa kupitishwa na kuthibitishwa,

iii. Kutayarisha taarifa za fedha za benki kwa ajili ya ukaguzi na kuziwasilisha kwenye Kamati Elekezi ya mkoa ili kuzipitia, kuzichambua na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mkoa kwa uthibitisho,

iv. Kusaidia utekelezaji wa mipango ya mkoa ya kila mwaka na mingineyo, programu na miradi/huduma kama itakavyoamuliwa,

v. Kutengeneza bajeti na kusimamia fedha za utekelezaji wa shughuli za kila siku za Sekretarieti ya mkoa,

vi. Kuandika na kuziweka pamoja taarifa kutoka wanachama wa mitandao wa mkoa kwa ajili ya kuzihifadhi na kuweka kumbukumbu,

vii. Kusimamia na kukagua fedha na vifaa vyote vya mtandao kwenye ngazi ya mkoa,

viii. Kuitisha vikao vyote vya Kamati Elekezi ya mkoa na Mikutano Mikuu ya mkoa baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa mwenyekiti wa Kamati Elekezi ya mkoa na pia kutunza mihtasari, taarifa na nyaraka zote,

ix. Kuhakikisha kwamba raslimali zote za Mtandao katika mkoa zinasimamiwa na kutumiwa ipasavyo kulingana na sera, kanuni na taratibu za Mtandao,

x. Kuhakikisha kuwa vitabu vyote vya hesabu vya Mtandao kwenye ngazi ya mkoa vinatunzwa ipasavyo

8.0 IBARA YA NANE: Mikutano

8.1.0: Mkutano Mkuu wa Taifa / Mkoa

i. Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa/Mkoa utakaofanywa mara moja katika kipindi kisichozidi miezi ishirini na minne (24) ambao utajulikana kama mkutano mkuu wa kawaida. Pia,

ii. Kutakuwa na mikutano isiyo ya kawaida itakayoitishwa wakati wowote itapohitajika na itajulikana kama mikutano ya dharura,

iii. Kamati Elekezi za Taifa na mkoa zitawakaribisha watazamaji, ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura, kuhudhuria mkutano wowote wa kawaida au wa dharura, pale itakapoonekana inafaa kulingana na mamlaka yatakayotolewa na Mkutano Mkuu wa Taifa/mkoa,

8.1.1: Taratibu za Uendeshaji wa Mikutano Mikuu ya Kawaida na Dharura

i. Mikutano yote mikuu (ya kawaida na dharura) itaitishwa na mratibu katika ngazi husika baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa mwenyekiti wa Kamati Elekezi katika ngazi husika. Au,

ii. Theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa mkutano mkuu katika ngazi husika kwa kutia sahihi waraka wa kusudio la kuitishwa kwa mkutano utakaofafanua sababu za kuitisha mkutano huo, na kumtaka mratibu kwa mujibu wa waraka huo aitishe mkutano mkuu usio wa kawaida, hali hii itatokea pale tu itakapoonekana kuwa taratibu za kawaida za uitishaji mikutano zimeshindikana,

iii. Taarifa ya Mkutano Mkuu itatolewa siku ishirini na moja kabla ikiambatanishwa na madhumuni na ajenda za mkutano,

iv. Taarifa ya mkutano mkuu wa dharura itatolewa siku kumi na nne (14) kabla ikiambatanishwa madhumuni na ajenda ya mkutano huo,

v. Katika mkutano mkuu wowote wa kawaida au wa dharura, theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wenye uanachama hai watatimiza akidi ambayo kama haikufikiwa hakutakuwa na shughuli/uamuzi utakaofanywa,

vi. Ikiwa akidi haitatimia baada ya muda wa kutosha kupita tangu muda uliopangwa kuanza kikao, mkutano utaahirishwa kwa uamuzi wa waliohudhuria; kwa vyovyote utaahirishwa kwa siku zisizopungua ishirini na moja na kufanywa tena mahali na wakati kama wa mwanzo au wakati na mahali pengine kama itakavyoamuliwa na Kamati Elekezi katika ngazi husika. Na,

vii. Ikiwa akidi haikutimia baada ya muda wa kutosha kupita tangu muda uliopangwa kuanza mkutano kwenye mkutano ulioahirishwa awali, wanachama waliohudhuria watatimiza akidi. Lakini,

viii. Hakuna jambo jipya litakalofanywa kwenye mkutano huu zaidi ya mambo yaliyoachwa kwenye mkutano ulioahirishwa,

ix. Kwenye vikao vyote vya Mkutano Mkuu, maamuzi yatafikiwa kwa kunyoosha mikono. Hata hivyo,

x. Itakubalika ikiwa mwanachama yeyote ataomba kuwe na kura ya siri kabla au baada tu ya kuhesabu kura ya kunyoosha mikono,

xi. Azimio la kupiga kura, kumteua au kumfukuza mwanachama yeyote litapitishwa kwa kura ya siri. Pia,

xii. Kupiga kura kwa kuwakilishwa kutakubaliwa kwenye Mikutano Mikuu. Uwakilishi huo utakubaliwa ukiwa kwa maandishi na kuwasilishwa kwa mwenyekiti kabla au wakati wa mkutano,

xiii. Pale ambapo kura zitafungana, ikiwa ni kwa kunyoosha mikono au kupiga kura ya siri, mwenyekiti wa mkutano husika atakuwa na haki ya kura ya pili au kura ya uamuzi.

8.2.0: Mikutano ya Kamati Elekezi za Mikoa na Taifa

i. Kamati Elekezi za mikoa na Taifa zitakutana kwa kawaida mara moja kila baada ya miezi sita (6). Hata hivyo,

ii. Mkutano wowote usio wa kawaida unaweza kuitishwa kukiwa na suala la dharura ama haraka,

iii. Kamati Elekezi za mkoa na Taifa zitawakaribisha watazamaji, ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura, kuhudhuria mkutano wowote wa kawaida au wa kawaida pale itakapooneka inafaa, kulingana na mamlaka itakayopewa na Mkutano Mkuu wa Taifa/ mkoa, .

8.2.2: Taratibu za Uendeshaji wa Mikutano ya Kamati Elekezi za mikoa na Taifa

i. Mikutano yote itaitishwa na mratibu baada ya kupata maelekezo kutoka kwa mwenyekiti wa Kamati Tedaji katika ngazi husika,

ii. Theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa mkutano wa Kamati Elekezi katika ngazi husika kwa kutia sahihi waraka wa kusudio la kuitishwa kwa mkutano utakaofafanua sababu za kuitisha mkutano huo, na kumtaka mratibu kwa mujibu wa waraka huo aitishe mkutano wa Kamati Elekezi usio wa kawaida; hali hii itatokea pale tu itakapoonekana kuwa taratibu za kawaida za uitishaji mikutano zimeshindikana,

iii. Taarifa ya kuitishwa mkutano wa Kamati Elekezi wa kila baada ya miezi sita (6) itatolewa siku saba (7) kabla ya mkutano,

iv. Taarifa ya mkutano wowote usio wa kawaida itatolewa kwa kipindi kifupi ikibidi chini ya saa 24 kulingana na mazingira ya dharura,

v. Mikutano yote itakayoitishwa kwa kuzingatia ibara 8.2.2 (a) itaendeshwa na mwenyekiti wa Kamati Elekezi katika ngazi husika, na endapo hatakuwepo makamu wake atafanya kazi hiyo. Lakini,

vi. Mkutano wowote utakaofanywa kwa kuzingatia ibara 8.2.2 (b) utaendeshwa na mjumbe yeyote wa Kamati Elekezi katika ngazi husika atakayeteuliwa na wajumbe kwa ajili ya kikao hicho tu,

vii. Kwenye mkutano wowote wa kawaida au usio wa kawaida nusu (1/2) ya wajumbe wa Kamati Elekezi katika ngazi husika watatimiza akidi ambayo kama haikutimia hakutakuwa na jambo/uamuzi utakaoweza kufanywa,

viii. Katika mikutano yote ya Kamati Elekezi, uamuzi utafikiwa kwa kunyoosha mikono. Hata hivyo,

ix. Itakubalika iwapo mjumbe yeyote ataomba kura ya siri kabla ama baada tu ya kura ya kunyoosha mikono kuhesabiwa,

x. Uamuzi wa kupiga kura, kumteua au kumfukuza mwanachama yeyote utapitishwa kwa kura ya siri. Pia,

xi. Upigaji kura kwa kuwakilishwa utakubaliwa kwenye Kamati Elekezi. Uwakilishi huo utakubaliwa ukiwa kwa maandishi na kuwasilishwa kwa mwenyekiti kabla ama wakati wa mkutano,

xii. Pale ambapo kura zitafungana, ikiwa ni kwa kunyoosha mikono au kupiga kura ya siri, mwenyekiti wa mkutano husika atakuwa na haki ya kura ya pili au kura ya uamuzi.

9.0 IBARA YA TISA Kazi na sifa za viongozi

Mtandao utakuwa na viongozi wafuatao; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti,, Mratibu.

9.1.0 MWENYEKITI

(i) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu.

(ii) Ataongoza Mtandao kwa kipindi cha miaka 3

(iii) Anaweza kuchaguliwa kwa awamu mbili mfululizo.

(iv) Anaweza kuchaguliwa tena kushika wadhifa huo baada ya kutoka madarakani awamu moja.

9.1.1 Sifa za Mwenyekiti

(i) Awe Mwanachama hai

(ii) Awe na umri wa miaka 25(ishirini na tano) na kuendelea

(iii) Awe na kiwango cha elimu kitakachomwezesha kusimamia kikamilifu shughuli za mtandao

(iv) Awe na uwezo wa kuongea kwa ufasaha Kiswahili na Kiingereza.

(v) Awe na ujuzi na uzoefu katika uongozi

(vi) Awe mzoefu katika shughuli za malezi, makuzi na maendelo ya watoto wadogo angalau kwa miaka mitatu.

9.1.2: Kazi za Mwenyekiti

(i) Ataongoza vikao vyote vya Kamati Elekezi na mkutano mkuu wa Taifa isipokuwa Mkutano Mkuu wa uchaguzi.

(ii) Kwa kushirikiana na Katibu Mtendaji wa mtandao wataitisha vikao vyote ngazi ya Taifa

(iii) Atakuwa muidhinishaji wa fedha

(iv) Atafuatilia mapato na matumizi ya mtandao

(v) Atasimamia na kutetea katiba ya mtandao.

9.1.3 Makamu Mwenyekiti

i. Atachaguliwa na Mkutano Mkuu katika ngazi husika

ii. Sifa na kazi za Makamu Mwenyekiti zitalingana na sifa za Mwenyekiti katika ngazi husika kama zilivyoainishwa katika ibara za 9.1.0, 9.1.1, 9.1.2 za katiba hii

iii. Makamu Mwenyekiti atafanya kazi atakazopewa na Mwenyekiti au kufanya kazi za mwenyekiti ikiwa mwenyekiti hayupo.

9.2.0. MRATIBU

9.2.1 Sifa za Mratibu

(i) Atakuwa mwajiriwa wa mtandao

(ii) Awe na umri usiopungua miaka 25

(iii) Awe na uzoefu katika shughuli za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo

(iv) Pamoja na sifa zitakazoainishwa katika taratibu za ajira yake.

9.2.2 Kazi za Mratibu

(i) Atafanya fanya kazi zote za ukatibu

(ii) Atafanya kazi zote za utendaji

(iii) Atafanya kazi zote za uratibu

(iv) Atawajibika kwa Kamati Elekezi

(v) Atafanya mawasiliano yote kati ya mtandao, taasisi, serikali na vyama vingine, mashirika mengine ndani na nje ya nchi.

(vi) Atakuwa msemaji mkuu wa Mtandao katika kazi za siku kwa siku.

(vii) Atakuwa msimamizi wa raslimali watu na fedha.

(viii) Atafanya kazi zingine zote atakazopangiwa na mwajiri.

10.0 IBARA YA KUMI: Vyanzo vya Mapato

Fedha za Mtandao zitatokana na:

i. Ruzuku na ufadhili,

ii. Viingilio na ada za wanachamana za kila mwaka,

iii. Mapato kutokana na mali/miliki za Mtandao,

iv. Fedha zozote zitakazopatikana kutoka vyanzo vingine vinavyoruhusiwa kisheria.

11.0 IBARA YA KUMI NA MMOJA: Uthibiti wa fedha

11.1.0: Udhibiti wa Fedha

i. Fedha zote za Mtandao zitawekwa benki itakayoamuliwa/zitakazoamuliwa na Kamati Elekezi na isipoelekezwa vinginevyo, zitatolewa kwa hundi zitakazoidhinishwa na watia saini walioteuliwa na Kamati Elekezi kulingana na mamlaka ya jumla au maalumu kwa mujibu wa kanuni za usimamizi wa fedha.

12.0 IBARA YA KUMI NA MBILI: Mabadiliko ya katiba

12.1 Katiba hii inaweza kubadilishwa kwa kufanyiwa marekebisho kwenye vipengele vitakvyoonekana vinahitaji kuboreshwa ili kuleta tija kwa mtandao.

12.2 Hoja ya mapendekezo ya mabadiliko ya katiba itatakiwa kupitishwa na theruthi mbili za wajumbe wa mkutano mkuu wa mtandao.

12.3 Wanachama wote wa mtandao watahusika katika mchakato mzima wa mabadiliko ya katiba.

12.4 Mapendekezo ya katiba yatajadiliwa na Kamati huru itakayo toa mapendekezo kwa Kamati Elekezi ya Taifa itakayoyapitisha na kuyawasilisha kwenye mkutano mkuu wa Taifa.

12.5 Mkutano mkuu ndiyo utakaothibitisha na kupitisha mabadiliko ya katiba.

14.0 IBARA YA KUMI NA TATU: Kukoma/kuvunjika kwa matandao,

Mtandao utavunjika kwa azimio litakalopitishwa na theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu waliohudhuria kikao kilichoitishwa maalumu kwa madhumuni hayo.

Kamati Elekezi itateua Mfilisi kuhakikisha kuwa mali za Mtandao zinatumiwa kulipa madeni ya Mtandao.

Ziada yoyote itakayobaki itakabidhiwa kwa mbia/mshiriki yeyote anayefanya shughuli zinazofanana na zile za Mtandao wa Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania.

15.1. IBARA YA KUMI NA NNE: Hitimisho/makubaliano.

Makubaliano ya katiba hii yamefanywa na mkutano mkuu wa TECDEN mbele ya wajumbe 45 (arobaini na watano) kama ilivyoorodheshwa kwenye Muhtsari.

Sahihi ya mwenyekiti_____ Sahihi ya Katibu_____

Tarehe _____ Tarehe _____